


## UTABIRI WA MVUA ZA *MSIMU* (NOVEMBA, 2023 – APRILI, 2024)



**Kielelezo 1. Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024)**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

## **Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2023 – Aprili, 2024)**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za *Msimu* kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

### **a) Mwelekeo wa mvua za *Msimu* kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:**

- (i) Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Iringa, Lindi, Mtwara, Singida, Dodoma, kaskazini mwa mkoa wa Katavi, Kigoma na Tabora. Aidha, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa kusini mwa mkoa wa Katavi, mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya na Ruvuma.
- (ii) Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2023 katika maeneo ya magharibi na kutawanyika katika maeneo mengine mwezi Novemba, 2023.
- (iii) Kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2023 – Januari, 2024) kinatarajiwa kuwa na mvua nyingi ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari – Aprili, 2024).
- (iv) Uwepo wa El-Niño unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mvua za *Msimu*.

### **b) Athari na ushauri**

- (i) Shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo.
- (ii) Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka.
- (iii) Wadau mbalimbali wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali maji.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

# **1. MWENENDO WA MVUA ZA VULI, 2023 NA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2023 HADI APRILI, 2024)**

## **1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023**

Msimu wa Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2023 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) pamoja na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba)) utabiri wake ulitolewa tarehe 24 Agosti, 2023. Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zilitarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini na ukanda wa Ziwa Victoria. Aidha, kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na maeneo machache ya mashariki mwa Ziwa Victoria mvua zilitarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani.

Mvua hizo zimeshaanza katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, pwani ya kaskazini na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki kama ilivyotabiriwa. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika miezi ya Novemba na Disemba, 2023. Vilevile, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika mwezi Januari na Februari, 2024.

## **1.2 Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024)**

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Iringa, Lindi, Mtwara, Singida, Dodoma, kaskazini mwa mkoa wa Katavi, Tabora na Kigoma. Aidha, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya, Ruvuma na kusini mwa mkoa wa Katavi. Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa na vipindi vya ukavu hususan mwezi Februari, 2024. Aidha, hivyo, mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2023 – Januari, 2024) ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari – Aprili, 2024). Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

### **i. Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):**

Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora na kaskazini mwa mkoa wa Katavi. Kwa maeneo ya kusini mwa mkoa wa Katavi, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba na ya kwanza ya mwezi Novemba, 2023 katika maeneo mengi na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2024.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

**ii. Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):**


Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Juu ya Wastani hadi Wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2023 na kuisha wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2024.

**iii. Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya na Njombe. Aidha, mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mkoa wa Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2023 na kuisha wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2024.

**iv. Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma):**

Mvua zinatarajiwa kuwa za Juu ya Wastani hadi Wastani katika mikoa ya Lindi na Mtwara; na Wastani hadi Juu ya Wastani katika mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2023 katika mikoa ya Lindi na Mtwara; na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2023 kwa mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2024 kwa mikoa ya Lindi na Mtwara; na wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2024 kwa mkoa wa Ruvuma.



**Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2023 –Aprili, 2024) na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Msimu (1991-2020).**

**Angalizo:** Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## **2. MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto la Bahari katika eneo la kati la kitropiki la bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la juu ya wastani katika kipindi cha Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024. Hali hii inaashiria kuendelea kuwepo kwa hali ya El-Niño. Hata hivyo, hali ya El-Niño inatarajiwa kupungua nguvu kadiri tunavyoelekea mwisho wa msimu wa mvua. Kwa upande wa Bahari ya Hindi, hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa kuendelea kuwepo upande wa magharibi mwa bahari kwa msimu wote wa mvua za Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024. Hali kadhalika joto la bahari la chini ya wastani hadi wastani linatarajiwa kuendelea kuwepo kwa upande wa mashariki mwa Bahari ya Hindi, hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu. Hali hii inaashiria kuendelea kuwepo kwa hali inayotambulika kama “Positive Indian Ocean Dipole (IOD)” katika nusu ya kwanza ya msimu wa mvua na baadae kupungua nguvu katika nusu ya pili ya msimu (Februari hadi Aprili, 2024). Kwa upande wa Bahari ya Atlantiki, joto la bahari la wastani hadi Juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari.

Kwa ujumla hali hii inatarajiwa kuimarisha mifumo inayosababisha mvua nchini hasa kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu.

Kwa upande mwingine, upepo kutoka misitu ya Kongo kuelekea nchini unatarajiwa kuimarika hasa katika nusu ya kwanza ya msimu. Hali hii inatarajiwa kuimarisha makutano ya upepo katika maeneo ya kati na mashariki mwa nchi, hali itakayochangia kuimarisha mifumo isababishayo mvua nchini.

## **3. ATHARI NA USHAURI**

Athari na ushauri umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 27 Oktoba, 2023.

### **a) Kilimo na Usalama wa Chakula**

Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo. Magonjwa kama vile ukungu (Fungus) yanatajariwa kuongezeka na kuathiri mazao kama viazi mviringo, nyanya, ufuta na maharage. Hata hivyo, shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, na kuchagua mbegu na mazao sahihi kwa ajili ya msimu huu. Aidha, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo pamoja na uvunaji maji ya mvua na kudhibiti visumbufu vya mimea ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)



## **b) Mifugo na Uvuvi**

Wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kufaidika na upatikanaji wa malisho, maji na chakula cha samaki. Hata hivyo, milipuko ya magonjwa ya mifugo kama vile ugonjwa wa homa ya bonde la ufa, midomo na kwato, na kuzaliana kwa wadudu wanaosambaza magojwa inaweza kujitokeza. Vilevile, matukio ya kuongezeka kwa magonjwa ya mwani baharini na kupungua kwa uzalishaji wa mwani kutokana na kupungua kwa kiwango cha chumvi ya maji ya bahari vinatarajiwa. Aidha, uharibifu wa mabwawa ya samaki kutokana na ongezeko la mvua unaweza kujitokeza.

Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Jamii inashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi bora ya maji na malisho. Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mwani kwenye maji ya kina kirefu ili kuondokana na athari za maji ya mvua yanayokuwa yanaingia baharini. Aidha, Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia mirejeo ya tabiri za hali ya hewa na ushauri kutoka kwa maafisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

## **c) Utalii na Wanyamapori**

Hali ya malisho na maji kwa ajili ya wanyamapori katika mbuga na hifadhi inatarajiwa kuwa nzuri. Hata hivyo, wingi wa mvua unaotarajiwa katika maeneo mengi unaweza kusababisha kutuama na kusambaa kwa maji na kupelekea wanyamapori kuhama, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani. Hali hii inaweza kusababisha magonjwa ya wanyamapori kusambaa kwa wanyama wanaofugwa na binadamu kutokana na wanyamapori kuingia katika makazi ya jamii zinazozunguka hifadhi na mbuga. Pia, hali hii inaweza kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa kutokana na kushambuliwa na wanyama wakali.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Hivyo basi, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika iwapo wanyamapori wataingia katika makazi au maeneo mbalimbali ya watu.

## **d) Usafiri na Usafirishaji**

Kutokana na utabiri huu, miundombinu ya usafiri na usafirishaji inaweza kuathirika hususan maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Juu ya Wastani. Matukio ya hali mbaya ya hewa yanaweza kuharibu miundombinu ya barabara na reli, ongezeko la ajali barabarani katika usafiri wa nchi kavu (barabara na reli); kuchelewa au kusitishwa kwa safari za ndege na reli; mawasiliano hafifu angani na majini; na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji katika shughuli za usafiri na usafirishaji kwa ujumla. Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

### **e) Nishati, Maji na Madini**

Upatikanaji wa maji unatarajiwa kuimarika, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani na Juu ya Wastani. Kina cha maji katika mabwawa, maziwa na mito kinatarajiwa kuongezeka. Hivyo, athari katika miundombinu ya rasilimali maji, usambazaji maji, uchimbaji mdogo wa madini na nishati inaweza kujitokeza. Shughuli za uchimbaji madini hususan katika migodi midogo zifanyike kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi.

Wadau wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali maji katika shughuli za uchakataji wa madini, uzalishaji wa umeme, matumizi ya viwandani na majumbani. Hali kadhalika, mamlaka husika zinashauriwa kuimarisha miundombinu ya rasimali za maji na kuweka mipango madhubuti ya uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka vyanzo mbadala kama vile nishati ya jua, jotoardhi, upepo na gesi endapo kutatokea uharibifu wa miundombinu kutokana na athari za mvua za Juu ya Wastani.

### **f) Mamlaka za Miji na Wilaya**

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za Miji na Wilaya zinashauriwa kuboresha mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Kamati za Usimamizi wa Maafa ngazi za kijiji na Wilaya ili ziweze kujiandaa, kukabiliana na kupunguza athari pindi zitakapotokea.

### **g) Sekta ya Afya**

Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji taka unaoweza kusababishwa na maji kutuama na kutiririka. Hivyo, jamii inashauriwa kuchukua hatua kuhakikisha usafi wa mazingira yanayowazunguka, kuharibu mazalia ya mbu na kudumisha usafi kwa ujumla. Mamlaka za afya zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kupunguza athari zinazoweza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kutumia, pamoja na kunywa maji safi na salama. Pia, kuhakikisha uwepo wa dawa za kutosha katika vituo vya afya kwa kuzingatia uwezekano wa uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji.

### **h) Sekta Binafsi**

Shughuli za kilimo na uzalishaji viwandani zinatarajiwa kunufaika kutokana na mvua za kutosha zinazotarajiwa katika msimu huu. Hata hivyo, wingi wa mvua unaweza kupelekea athari katika shughuli za ujenzi wa miundombinu, uhifadhi na usafirishaji wa mazao tete na bidhaa.

Wadau wa Sekta Binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

### **i) Menejimenti za Maafa**

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani vipindi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi na kupelekea uharibifu wa miundombinu, mazingira, upotevu wa mali na madhara kwa binadamu. Hivyo, Idara ya Menejimenti ya Maafa nchini inashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango itakayosaidia kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, sekta, mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha kuzuia au kupunguza madhara.

### **j) Vyombo vya Habari**

Vyombo vya habari vinashauriwa kupata utabiri, kufuatilia na kusambaza taarifa na tahadhari za hali ya hewa pamoja na zile zilizo huishwa na Mamlaka. Vyombo vya habari pia vinashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kissekta kutoka sekta husika wakati wa kuandaa na kutoa taarifa mtambuka za hali ya hewa kwa jamii. Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa na kusambaza makala za kitaalamu kwa kutumia lugha nyepesi kwa lengo la kuhabarisha jamii juu ya matumizi sahihi ya utabiri wa hali ya hewa. Vilevile, kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika kuandaa vipindi maalum vya kutoa elimu na kwa wakati kuhusu athari mbalimbali za hali ya hewa zinazotarajiwa kutokea na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na athari hizo.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahususi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

**Imetolewa: 31 Oktoba, 2023**

**Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

---

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)  
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)